*Tangazo la Serikali Na.127 (linaendelea)*

WHEREAS, the Government has deemed to be appropriate that certain assets of the National Agricultural and Food Corporation be vested to the Ministry of Works of the United Republic of Tanzania (Tanzania Building Agency);

NOW THEREFORE, It is hereby directed as follows:-
The assets of the National Agricultural and Food Corporation specified in the Schedule hereto shall, vest, without further assurance, to the Ministry of Works of the United Republic of Tanzania (Tanzania Building Agency).

SCHEDULE

House on Plot No. 540, Block "F" (B. 13), Msasani-Drive (in) Dar es Salaam

BY COMMAND OF PRESIDENT

Dar es Salaam,
6th December, 2004

MATETN Y. C. LUMBANGA
*Chief Secretary*

TANGAZO LA SERIKALI NA 128 la tarehe 13/5/2005

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
1982

(NA. 7 YA 1982)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 148*

SHERIA NDOGO (HIFADHI YA MAZINIGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA, 2004

Jina 1. Sheria hizi zinaitwa Sheria Ndogo (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, 2004.





*Tangazo la Serikali No. 128 (linaendelea)*

2. Katika Sheria Ndogo hizi:- Tafsiri

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa;
"kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti, visiki, vichaka na majani;
"maeneo ya hifadhi" maana yake ni pamoja na vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, maeneo ya mteremko na maeneo mengine yatakayotangazwa kuwa ya hifadhi;
"mazao ya misitu" ni pamoja na mbao, fito, miti, mkaa, kuni na mbegu za miti na mazao mengine ya misitu;
"misitu" maana yakie ni uoto wa asili au wa kupandwa na ni pamoja na miti, vichaka, majani na nyasi au vyote kwa pamoja ulioko ndani ya eneo la Halmashauri;
"sehemu ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri au Halmashauri ya Kijiji kulishia mifugo.

3.-(1) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kuchoma moto au kusababisha kuchoma moto kwa namna yoyote ile katika eneo bila kuomba na kupata idhini kutoka Halmashauri au Halmashauri ya Kijiji. Kuzuia kuchoma moto

(2) Mtu yeyote atakayetaka kuchoma moto kwa madhumuni ya kilimo atatakiwa kuomba na kupata kibali kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji baada ya kupata maoni na mapendekezo kutoka kwa mwenyekiti wa kitongoji ambaye atatakiwa kukagua eneo hilo kabla ya kupendekeza kutolewa kwa kibali hicho.

(3) Kibali ambacho kitatolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analitaka kuchoma moto.

(4) Muda wa kuchoma moto kwa madhumuni ya Sheria Ndogo hizi ni majira ya alfajiri au jioni na ni wajibu wa mchomaji wa eneo kuzungushia barabara ya kuzuia moto *(fire breaks)* ili moto usiingie sehemu isiyohusika.

4.-(1) Ni wajibu wa kila Mwenyekiti wa Kitongoji, kijiji na Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata kutoa amri ya kwenda kuzima moto unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha na mali za watu, na uharibifu wa mazingira katika eneo analoongoza. Wajibu wa Viongozi wa Serikali